أَحَادِيثُ ضَعِيفَةٌ تَتَعَلَّقُ بِالأُضْحِيَّةِ

(مِنْ كِتَابِ سِلْسِلَةِ أَحَادِيثِ الضَّعِيفَةِ)

HADITHI DHAIFU ZINAZOFUNGAMANA NA UDH-HIYA

(KUTOKA KWENYE KITABU SILSILAT AHAADITHI DDHA'IIFA)

Mwandishi:

Abu Halima Arafaat Bin Mahmoud

Utangulizi

Kila sifa njema anastahiki Allaah Mola Mlezi wa viumbe wote. Swala na Salamu Zimshukie Mtume wetu Muhammad, Jamaa zake na Maswahaba wake.

Baada ya hayo:

Ndugu msomaji, nataraji umejifunza mambo mengi na kufaidika kupitia Makala yetu tuliyoiandika kuelezea baadhi ya hukumu za mnyama wa Udh-hiya.

Katika ukamilifu wa faida kuhusiana na maudhui hii, nimeona niandike Makala hii fupi katika kubainisha hadithi dhaifu zenye kufungamana na mnyama wa Udh-hiya, kwa sababu watu wengi huzitumia hadithi hizi kwa ajili ya kuhimiza juu kutekeleza ibada hii, huenda kwa sababu ya kutojua kwamba hazijathibiti kutoka Mtume ﷺ na wala hazifai kuzitumia kuwa ni hoja katika jambo hili, na badala yake zipo hadithi sahihi amabzo zinatosheleza kuelezea na kufafaunua Ibada hii tukufu ya Udh-hiya.

Ndugu msomaji, hizi ni hadithi saba, zipo katika hizo hadithi dhaifu na nyingine ni maudhuu' (hadithi za kutunga), zote hizo hazifai kuzitumia katika jambo hili la Udh-hiya, hadithi hizi zimechukuliwa ndani ya kitabu **[Silsilat Aadiithi Ddha'iifa]** cha Sheikh Muhammad Nasiru Ddiin رَحِمَهُ اللهُ .

Tunamuomba Allaah aweke Taufiq na Qabul katika amali yangu hii na atujaalie ni katika watu wenye kufuata mwongozo sahihi wa Dini yake.

Abu Halima Arafaat Bin Mahmoud

بسم الله الرحمن الرحيم

1.

«مَا عَمِلَ ابْنُ آدَمَ فِيْ هَذَا اليَوْمِ أَفْضَلَ مِنْ دَمٍ يُهْرَاقُ، إِلَّا أَنْ تَكُوْنَ رَحِمًا تُوْصَلُ»

“Hajafanya mwanadamu amali yoyote bora zaidi katika siku hii (ya Eidul Adh-ha) kuliko damu inayomwagwa (mnyama wa Udh-hiya), isipokuwa kuunga udugu”[1].

2.

«مَا عَمِلَ آدَمِيٌّ مِنْ عَمَلٍ يَوْمَ النَّحْرِ أَحَبَّ إِلَى اللهِ مِنْ إِرْهَاقِ الدَّمِ، إِنَّهُ لَيَأْتِي يَوْمَ القِيَامَةِ بِقُرُوْنِهَا وَأَشْعَارِهَا وَأَظْلَافِهَا، وَإِنَّ الدَّمَ لَيَقَعُ مِنَ اللهِ بِمَكَانٍ قَبْلَ أَنْ يَقَعَ عَلَى الأَرْضِ، فَطَيِّبُواْ بِهَا نَفْسًا»

“Hajafanya mwanadamu amali yoyote siku ya (Eid ya) kuchinja (amali) inayopendeza zaidi mbele ya Allaah kuliko kumwaga damu (kuchinja mnyama wa Udh-hiya), hakika atakuja (mnyama huyo) siku ya kiama akiwa pamoja na pembe zake, manyoya na kwato zake, na hakika damu inayoanguka mbele ya Allaah (kwa ajili ya kumridhisha yeye) ni yenye kukubaliwa kabla ya kuanguka juu ya ardhi, basi zisafisheni kwa ajili ya (mnyama) huyo nafsi zenu”[2].

Amesema Ibnul Malak رَحِمَهُ اللهُ wakati akifafanua hadithi hii:

"أَيْ إِذَا عَلِمْتُمْ أَنَّهُ تَعَالَى يَقْبَلُهُ وَيَجْزِيكُمْ بِهَا ثَوَابًا كَثِيرًا فَلْتَكُنْ أَنْفُسُكُمْ بِالتَّضْحِيَةِ طَيِّبَةً غَيْرَ كَارِهَةٍ لَهَا"

“Maana yake: Mkiwa mnafahamu kwamba (yeye) Allaah Ta’alaa anampokea (mnyama huyo) na kuwalipa nyinyi ujira mwingi kwa sababu yake, basi ziwe nafsi zenu ni nzuri (zimeridhika) kwa ajili ya kujitolea (kuchinja Udh-hiya), na wala zisiwe zenye kuona karaha (kuchukia)”[3].

3.

«الأَضَاحِيُّ سُنَّةُ أَبِيْكُمْ إِبْرَاهِيْمَ، قَالُواْ: فَمَا لَنَا فِيْهَا؟ قَالَ: بِكُلِّ شَعْرَةٍ حَسَنَةٌ، قَالُواْ: فَالصُّوْفُ؟ قَالَ: بِكُلِّ شَعْرَةٍ مِنَ الصُّوْفِ حَسَنَةٌ»

1- Kitabu: [Silsilat Ahaadiithi Ddha’iifa] (Jz. 2, Uk. 13) hadithi namba (525).
2- Kitabu: [Silsilat Ahaadiithi Ddha’iifa] (Jz. 2, Uk. 14) hadithi namba (526).
3- Kitabu: [Tuhfatul Ahwadh] (Jz. 5, Uk. 62).

“Udh-hiya ni sunna ya baba yenu Ibrahim, wakauliza: je ni kiasi gani cha thawabu tunachopata katika (kuchinja) Udh-hiya? Akasema: (mtapata) badali ya kila unywele/nyoya moja thawabu za (kutenda) wema mmoja, wakauliza: je Sufi (manyoya ya kondoo)? Akasema: (mtapata) badali ya kila unywele/nyoya moja la Sufi thawabu za (kutenda) wema mmoja”[4].

Kwa sababu neno: (شَعْرَة – sha’ra) hutumika kwa manyoya ya mbuzi tu, ndio maana Maswahaba رَضِيَ اللهُ عَنْهُمْ wakamuuliza tena Mtume ﷺ kuhusu manyoya ya kondoo (الصُّوْفُ – Sufi), je nayo watapata kiasi gani cha ujira? Mtume ﷺ akawajibu sawa na alivyowajibu kuhusiana na manyoya ya mbuzi, kama vile neno (وَبَرٌ – wabar) hutumika kwa manyoya ya ngamia.

4.

«يَا فَاطِمَةُ قَوْمِي إِلَى أُضْحِيَّتِكِ فَاشْهَدِيْهَا فَإِنَّهُ يُغْفَرُ لَكِ عِنْدَ أَوَّلِ قَطْرَةٍ تَقْطُرُ مِنْ دَمِهَا كُلُّ ذَنْبٍ عَمِلْتِيْهِ وَقُولِيْ: ﴿إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ﴾ »

“Ewe Fatma, simama ukashuhudie mnyama wako wa Udh-hiya na useme: “Hakika Swala zangu, Kuchinja kwangu, Uhai wangu na Kufa kwangu, (yote hayo) ni kwa ajili ya Allaah”. kwani hakika utasamehewa wewe kila dhambi uliyoifanya kwa tone la kwanza lenye kudondoka katika damu yake”[5].

Hadithi hii ni Munkar: mpokezi wake ni mtu dhaifu, haikubaliwi hadithi akipokea peke yake au akiwa amesimulia tafauti na alivyopokea mtu muaminifu, mwenye kudhibiti (Thiqat).

5.

«مَنْ ضَحَّى طَيِّبَةً بِهَا نَفْسُهُ، مُحْتَسِبًا لِأُضْحِيَّتِهِ؛ كَانَتْ لَهُ حِجَابًا مِنَ النَّارِ»

4- Kitabu: [Silsilat Ahaadiithi Ddha’iifa] (Jz. 2, Uk. 14) hadithi namba (527).
5- Kitabu: [Silsilat Ahaadiithi Ddha’iifa] (Jz. 2, Uk. 15) hadithi namba (528).

“Atakaechinja mnyama wa Udh-hiya kwa kuridhika nafsi yake, na kutarajia thawabu kwa kichinjwa chake hicho, (basi) kitakuwa (kichinjwa hicho) ni kinga yake na moto (siku ya kiama)”[6].

6.

«نَسَخَ الْأَضْحَى كُلَّ ذَبْحٍ، وَصَوْمُ رَمَضَانَ كُلَّ صَوْمٍ، وَالْغُسْلُ مِنَ الْجَنَابَةِ كُلَّ غُسْلٍ، وَالزَّكَاةُ كُلَّ صَدَقَةٍ»

“Amefuta (mnyama wa) Udh-hiya kila kichinjwa cha wajibu, na (imefuta) Saumu ya ramadhani kila saumu ya wajibu, na (limefuta) josho la janaba kila josho la wajibu, na (imefuta) Zaka kila sadaka ya wajibu”[7]. Hadithi hii ni dhaifu sana.

Maana yake ni kwamba: Hakuna kichinjwa kingine cha wajibu zaidi ya Udh-hiya, kwa hiyo hadithi hii inafahamisha juu ya kwamba kuchinja Udh-hiya ni wajibu, kadhalika hukumu ni kama hivyo kwenye Saumu ya ramadhani, Josho la janaba na Zaka, vyote hivyo vimefuta vilivyo chini yake, hadithi hii ni dhaifu sana wala haifai kuifanya kuwa ni hoja.

7.

«إِنَّ أَفْضَلَ الضَّحَايَا أَغْلَاهَا وَأَسْمَنُهَا»

“Hakika mnyama bora wa Udh-hiya ni mwenye thamani kubwa (ghali) na aliye mnene”[8].

Swala na Salamu Zimshukie Mtume wetu Muhammad ﷺ

Wabillaahi Ttaufiiq

Abu Halima Arafaat Bin Mahmoud

Pongwe Tanga

06/Dhul-Hijjah/12/1443ᴴ – 05/07/2022ᴹ

Simu: 0715263253

6- Kitabu: [Silsilat Ahaadiithi Ddha’iifa] (Jz. 2, Uk. 15) hadithi namba (529).
7- Kitabu: [Silsilat Ahaadiithi Ddha’iifa] (Jz. 2, Uk. 304) hadithi namba (904).
8- Kitabu: [Silsilat Ahaadiithi Ddha’iifa] (Jz. 4, Uk. 174) hadithi namba (1678).